NA. MK 01

(Kupangisha Vyumba / Fremu)

SHERIA YA ARDHI
(NA. 4 YA 1999)

# CHAMA CHA MAPINDUZI

MKOA WA ..Arusha......................................................

(OFISI YA CCM ..................................................)

MKATABA WA KUPANGISHA

BAINA YA

BARAZA LA WADHAMINI WA CHAMA CHA MAPINDUZI
(MPANGISHAJI)

NA

Mtei Express Coach LTD
(MPANGAJI)

CHAMA CHA MAPINDUZI ... WA ARUSHA

## MKATABA WA KUPANGISHA

MKATABA HUU WA KUPANGISHA umefanyika leo tarehe ....02.......... mwezi 01 mwaka 2017

BAINA YA

BARAZA LA WADHAMINI WA CHAMA CHA MAPINDUZI wa S.L.P 50 Dodoma likiwa limeundwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258 na kusajiliwa chini ya Sheria ya Wadhamini, Sura 318 R.E. 2002 (hapa litajulikana kama "Mpangishaji") kwa upande mmoja.

NA

Mtei Express Coach Ltd wa S.L.P 14320 Tel: 0754-264570........................ (hapa atajulikana kama " Mpangaji" ) kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mpangishaji ambaye ndiye mmiliki halali wa kiwanja nambari 57 Kitalu 'W' katika Levolosi - Kilombero Arusha.........

NA KWA KUWA Mpangaji anatafuta eneo la kupanga na yuko tayari kupanga.

HATI HII NI USHAHIDI wa mambo yafuatayo:-

1. Mpangishaji anampangisha Mpangaji fremu/chumba Jengo Mata / Yard....... kwa kipindi cha mwaka mmoja tu kutegemeana na kifungu cha 5(b) kuanzia tarehe ....01........ mwezi ..........Januari.......................: Mwaka....2017..................mpaka tarehe..............31..............mwezi Desemba.....mwaka 2017..........

2. Kodi itakuwa Tshs 2,000,000 (Milioni Mbili Tu) kwa mwezi na italipwa kwa malipo ya awali ( in advance) katika siku ya kwanza ya kila mwezi mmoja katika kipindi chote cha Mkataba huu. Malipo ya kwanza yamefanyika tarehe ......04........mwezi ....02.....mwaka ..2017.... kwa Mpagishaji.

3. MPANGAJI ANAKUBALI yafuatayo:-

   (a) Kulipa kodi ya pango kama iliyotajwa katika kifungu cha 2 hapo juu.

CHAMA CHA MAPINDUZI

(b) Kujilipia gharama za huduma za maji, umeme/ simu kwa kiwango kitakachoonyeshwa kwenye ankara.

(c) Kugharamia na kulipia uondoshaji wa maji machafu na taka katika eneo alilopangishwa.

(d) Wakati wote kulinda eneo alilopangishwa na maeneo yanayozunguka pamoja na milango, madirisha na vitu vilivyounganishwa kwenye eneo hilo, katika hali ya kuridhisha (isipokuwa uharibifu utakaosababishwa na majanga ya asili ambayo hayatokani na uzembe wake).

(e) Kutohifadhi au kutoleta katika Eneo lililopangishwa vitu vya aina yoyote ya mlipuko au vinavyoshika moto kwa urahisi au vitu vilivyo vya hatari vinavyoweza kuharibu jengo.

(f) Ataweka mazingira ya eneo lililopangishwa katika hali ya usafi kwa wakati wote wa upangaji wake na kutofanya au kutoruhusu kufanyika katika Eneo lililopangishwa jambo lolote au kitu chochote ambacho huenda kikasababisha usumbufu , uharibifu au kero kwa mpangishaji au Wakala wake, mpangaji mwingine au wakazi wa nyumba za jirani.

(g) Kutumia Eneo lililopangishwa kwa madhumuni ya aliyoomba tu na pindi ikitokea kubadili matumizi, itabidi Mpangaji aombe kwa barua na apate idhini ya maandishi kutoka kwa wa Mpangishaji au wakala wake.

(h) HATATOA au KUPANGISHA au KUKODISHA au KUONGEZA eneo lililopangishwa bila idhini ya maandishi kutoka kwa mpangishaji.

(i) Kurejesha eneo lililopangishwa pamoja na vitu vyote vilivyounganishwa katika hali ya kuridhisha kwa mujibu wa masharti ya mkataba mara au mapema baada ya kumalizika kipindi cha pango.

(j) Kuruhusu Mpangishaji au Wakala wake katika muda wote unaofaa na baada ya kutoa taarifa (notisi) kuingia kwenye eneo lililopangishwa kwa ajili ya kuangalia hali ya eneo hilo.

CHAMA CHA MAPINDUZI • MKOA WA ARUSHA •

MPANGISHAJI ANAKUBALI ...

a. Endapo Mpangaji atalipa kodi ya pango na kutimiza masharti na vipengele mbalimbali kwa upande wake, Mpangaji **ATAPANGA** na **KUTUMIA** eneo lililopangishwa kwa kipindi chote cha Mkataba bila kusumbuliwa ama kukatishwa na Mpangishaji au Wakala wake.

Taarifa yoyote inayotolewa kuhusiana na pango yaweza kutolewa na upande wowote kwa njia ya Posta kwa kutumia anwani ya Wakala wa Mpangishaji au Mpangaji au kwa njia ya mkono kadri itakavyokuwa inafaa ndani ya siku 7 tangu tarehe ya tukio na itahesabiwa kufika baada ya kulipia Posta/EMS.

**ISIPOKUWA**, hapa pande zote zinakubaliana na kutamka kama ifuatavyo:-

(a) Kodi iliyotajwa katika kifungu cha 2 katika mkataba huu itaongezeka kila baada ya miaka....Miwili....................ili kwenda sambamba na kupanda kwa gharama za uendeshaji ili mradi isipungue asilimia thelathini na tano (35%).

(b) Mkataba unaweza aidha kusitishwa na Mpangaji au Wakala wa Mpangishaji kwa kutoa taarifa (notisi) ya maandishi si chini ya siku thelathini (30) kwa upande mwingine.

(c) Mpangaji akishindwa kulipa kodi kwa miezi mitatu ama awamu nzima atakuwa kwa hiari yake amevunja mkataba huu hivyo atatakiwa kulipa limbikizo la kodi na kurudisha Eneo Lililopangishwa.

(d) Mpangaji akishindwa kulipa limbikizo la kodi (deni) na akakaidi kukabidhi Eneo Lililopangishwa, ikiwalazimu Wadhamini kuchukua hatua za kisheria za kulipwa kodi daiwa, gharama zote zitokanazo na uchukuaji wa hatua hizo za kisheria zitalipwa na Mpangaji.

(e) Inapotokea uharibifu wa Eneo Lililopangishwa kwa majanga ambayo hayatatokana na kosa la Mpangaji au Watumishi/ wageni wake, kodi au sehemu ya kodi hiyo itasitishwa kufuatana na kiwango cha uharibifu huo mpaka sehemu iliyoharibika itakapotengenezwa na kurekebishwa upya na kuwa ya kufaa kwa

CHAMA CHA MAPINDUZI MKOA WA ARUSHA

na kiwango cha uharibifu huo mpaka sehemu iliyoharibika itakapotengenezwa na kurekebishwa upya na kuwa ya kufaa kwa matumizi au makazi, kama hakuna matengenezo yatakayofanyika katika miezi sita (6), Mpangaji atakuwa na hiari ya kusitisha mkataba kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja.

(f) Kama Mpangaji anapenda kuendelea na mkataba huu baada ya kipindi cha mkataba kwisha, atatoa taarifa (notisi) ya maadishi ya miezi mitatu (3) kwa Wakala wa Mpangishaji, kabla ya kipindi cha mkataba kumalizika, KAMA taarifa (notisi) imetolewa na kutokubalika na Wakala wa Mpangishaji kwa maandishi, mkataba huu utakoma na malipo ya kodi kutoka kwa Mpangaji hayatapokelewa, na mpangaji atakayeendelea kukalia Eneo Lililopangishwa atahesabika kama mvamizi kuanzia tarehe ya ukomo wa mkataba.

(g) Pakitokea mgogoro wa tafsiri au kuhusu utekelezai wa mkataba huu (usiohusiana na kodi) ataitwa msuluhishi (arbitrator) anayekubalika na pande zote za mkataba na maamuzi yake yatakuwa ndiyo utatuzi wa mgogoro huo isipokuwa upande ambao hautaridhika na uamuzi wa msuluhishi unaweza kuupeleka mgogoro huu chini ya sheria ya Usuluhishi ((Arbitration Act, Cap. 15) mbele ya vyombo vya sheria.

KWA USHAHIDI HAPA, Katibu wa CCM Mkoa kwa niaba ya Kamati ya Siasa ya CCM ya Mkoa iliyoidhinishwa kisheria na Wadhamini kwa upande mmoja na Mpangaji kwa upande mwingine wamesaini mkataba huu tarehe na mwaka kama inavyoonekana hapa chini.

UMESAININIWA na KUTOLEWA na ....Daudi Daudi Billaly....
KATIBU WA CHAMA CHA MAPINDUZI ( M) WA ....Arusha....
KWA NIABA YA BARAZA LA WADHAMINI WA CHAMA CHA MAPINDUZI na KAMATI YA SIASA YA CCM MKOA ambaye namfahamu mimi binafsi/ametambulishwa kwangu na ................................ ambaye ninamfahamu mimi binafsi leo ametambulishwa kwangu na..........................tarehe ....02.........
Mwezi ............02......... mwaka ....2017.........

..............................
SAHIHI YA KATIBU WA CCM MKOA

Katibu wa CCM wa Mkoa
Arusha

yangu:

Jina: NEEMA BARNABA LUCUMAY

Sahihi: N.B.Lucumay

Anuani: 15806


ARUSHA

Wadhifa: Wakili/Hakimu

NEEMA BARNABA LUCUMAY
ADVOCATE
NOTARY PUBLIC
&
COMMISSIONER
FOR OATHS
P.O. Box 15806 ARUSHA

UMESAINIWA na KUTOLEWA na
NDERASIO N. MTEI
kwa niaba ya (Kampuni/ Taasisi)
MTEI EXPRESS COACH LTD
Ambaye ninamfahamu mimi binafsi/
Ametambulishwa kwangu na
..............................ambaye namfahamu
mimi binafasi leo tarehe ......02..........
mwezi .........02.......... mwaka ....2017...

PICHA YA MPANGAJI



SAHIHI YA MPANGAJI

Mbele yangu:

Jina: Emmanuel Laban Kilto

Sahihi:

Anuani: S.L.P 167, Moshi

..............................................................

Wadhifa: Wakili/~~Hakimu~~

EMMANUEL LABAN KILTO
ADVOCATE
NOTARY PUBLIC
&
COMMISSIONER
FOR OATHS
P.O. Box 167, MOSHI

UMETAYARISHWA NA:
Baraza la Wadhamini
Wa Chama Cha Mapinduzi
S.L.P 50,
DODOMA